



Yerusalemu Mpya

Mchungaji Tony Alamo

Makanisa Ulimwenguni Kote

Taifa la Kikristo la Alamo



Toleo 20500

NJIA PEKEE YA KUTOKEA

Na Tony Alamo



Tony Alamo kushoto na waongofu wapya wanaotarajiwu kubatizwa mwaka 1970

Mbegu ambayo MUNGU alimwambia Abrahamu kwamba itabariki mataifa yote ilikuwa ni mbegu yenne maisha yasiyo na kikomo ndani yake (Mwanzo 12:3). Mbegu zote zina maisha ya muda mfupi au mchache ndani yao, bali mbegu moja pekee ina uzima wa milele ndani yake na "mbegu hiyo ni NENO la MUNGU," ambalo ni YESU (Luka 8:11).¹ YESU ndiye mbegu pekee na pia ni mpanzi wa mbegu, NENO la MUNGU (Luka 8:5-15). Sisi tulio hekalu la MUNGU na Mwili wa KRISTO, Bibi arusi WAKE, tunaye YESU pamoja na BABA kwa ROHO aishiye ndani yetu, hivyo sisi nasi kwa ROHO tumekuwa wapanzi wa mbegu ya uzima wa milele, ambayo kwa mara nyingine ni KRISTO, aliye NENO (Yohana 4:36).²

Pia, sisi ni wale walioitwa kutoka ulimwenguni, kanisa.³ Tena, mbegu, YESU, ndiye NENO la MUNGU. Sisi, watakatifu, tulioitwa toka ulimwenguni, kanisa – vyote hivi ni uzima, uzima wa milele, ambao ni mbegu yenye kutokufa na tena, ni NENO la MUNGU, ambalo ni MUNGU aliyefanyika mwili akaishi

kati yetu, IMANUELI, ambalo lamaanisha. MUNGU yu pamoja nasi (Mathayo 1:23).

Baadhi ya wapumbavu husema, "Vema, najua kwamba sisomi Biblia kama ninavyotakiwa," wakidhani maneno haya ya kijinga wasemayo ni namna ya kujishusha na kunyenyeka, kukiri ukweli, na kwamba watajinasua kutoka kwenye kiopoo kwa kusema mambo haya ya kilegevu. Hata hivyo, wanajiumiza wenye milele. Kwa maana "imani huja kwa kusikia, na kwa kusikia NENO la MUNGU," ambalo ndilo mbegu, kitu pekee chenye uzima wa miele ndani yake (Warumi 10:17). NENO ni MUNGU (Yohana 1:1). MUNGU ni wa milele, hivyo kama MUNGU anaiishi ndani yako kwa utakatifu kupi-

tia kwa NENO, hutakufa kamwe, kama ukiendelea kuwa imara mpaka mwisho.⁴

Kila kitu tuonacho duni-ani kimefuliwa na NENO la MUNGU kutoka ard-hini, ili tuweze kuona wazi wazi, hasa wale tunaom-jua MUNGU au tuliowahi KUMFAHAMU.

"Kwa maana ghadhabu ya MUNGU imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu wapingao kweli kwa uovu. Kwa kuwa mambo ya MUNGU yanayo julikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana MUNGU aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo YAKE yasiyo onekana tangu kuumbwa kwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani uwezo WAKE wa milele na UUNGU wake; hata wasiwe na udhuru; kwa sababu walipomjua MUNGU [waliokuwa wakristo hapo awali] HAWAKUMTUKUZA kama ndiye MUNGU, wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; wakaubadili utukufu wa MUNGU asiye na uharibifu (Inaendelea ukurasa wa 2)

¹ Mat. 4: 3-4, Yoh. 1: 1, 14, 1 Yoh. 1: 1-3, 5:11, Ufu 19:13 ² Mk. 16: 15-16, 1 Kor. 1: 21-24, 6:19, 2 Kor. 5: 17-21 ³ Yoh. 15:16, 19, 17: 6, 14-16, 2 Kor. 6: 14-18, 1 Pet. 2: 9 ⁴ Mat. 4: 4, 10:22, 24:13, Yoh. 5:24, 6:63, 11:26, Mdo. 14:22, Rum. 11:22, Kol. 1: 22-23, 1 Tim. 4:16, 2 Tim. 2: 1-3, 3: 13-17, 4: 5, Yak. 5: 10-11, 1 Yoh. 2: 24-25

NJIA PEKEE YA KUTOKEA

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)

kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo.

“Kwa ajili ya hayo MUNGU aliwaacha katika tamaa za mioyo yao, waafuate uchafu, hata wakaivunja miili yao heshima. Kwa maana walibadili kweli ya MUNGU kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele. Amina. Hivyo MUNGU aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu, hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili; wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke, ya asili, wakawakiana tamaa, wanaume wakiyatenda yasiyopasa, wakapata naf-sini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao.

“Na kama walivyokataa kuwa na MUNGU katika fahamu zao, MUNGU aliwaacha wafuate aki-li zao zisizofaa, wayafanye yasi-yowapasa. Wamejawa na udhalimu wa kila namna, uovu na tamaa na ubaya; wamejawa na husuda, na uuaji, na fitina, na hadaa; watu wa nia mbaya, wenyewe kusengenya, wenyewe kusingizia, wenyewe kumchukia MUNGU, wenyewe jeuri, wenyewe

kutakabari, wenyewe majivuno, wenyewe kutunga mabaya, wasiowatii wazazi wao, wasio na ufahamu, wenyewe ku-vunja maagano, wasiopenda jamaa zao, wasio na mahaba asilia, wasio na rehemaa; ambaao wakijua sana hukumu ya haki ya MUNGU [kwa sababu kwa wakati fulani waliku-wa wameokoka], ya kwamba way-atendao hayo wamestahili mauti, wanatenda hayo, wala si hivyo tu, bali wanakubaliana nao wayatendao” (Warumi 1:18-32).⁵

Ulimwengu sasa umerudi na kufanana na ulimwengu ule wa siku za Nuhu (Mwanzo 6:5-7, Mat-thayo 24:37-44). Akili za watu leo zimebadili kweli ya MUNGU kuwa uongo (Warumi 1:21-25).⁶ MUNGU ndiye mbegu ya pekee YEYE ndiye mbegu pekee iliyo na uzima wa milele ndani YAKE. Na wanasema sasa, kama walivyosema nyakati za Nuhu, kwamba kweli hii ya MUNGU iliyo mbegu pekee ya uzima wa milele ni uongo, na wanafundisha watoto wetu upotovu huu mwovu na wa kuu-dhi katika shule zote za umma. Haiwatashi kuoana wenyewe kwa wenyewe. Wanataka kuwafundi-sha watoto wetu kwamba kweli ya MUNGU ni uongo. Wame-kubali mapepo (mapepo ya ushoga) ndani yao, mapepo imara yanayowafanya kuabudu mambo ambayo ni tamaa za mwili,

hivyo wanakitumikia kiumbe zaidi ya Muumba (Warumi 1:25). Kwa sababu hii, MUNGU anawaacha waende. AMEWAACHA wafuate tamaa mbaya, tabia zao wenyewe za tamaa zao mbaya, ambazo wanavyomkataa sana. MUNGU ana-onna jinsi walivyomkataa YEYE na uzima WAKE wa milele, kwa uovu wanapambana naye, kwa hiyo MUNGU hashughuliki nao tena. MUNGU amewaacha na kuwaruhusu kupata kile wanachotaka, ambacho ni kufuata tamaa zao mbaya za kuudhi! ANAWAACHA wafanye walichochagua kufanya – wanawake kwa wanawake, wanau-me kwa wanaume, usagaji na ushoga.

Hata hivyo, mbegu ya MUNGU, ya uzima wa milele, haitaishi katika

Nigeria

Mpendwa Mchungaji Tony,

Salamu kwako kwa jina la Yesu. Ninayo furaha kukwambia kwamba tayari nimekuwa mtumishi wa Mungu kuitia maandiko yako ya injili ninayosoma na kipindi chako cha redio katika Radio Africa. Nakushukuru kwa namna ambavyo unatangaza Neno la Mungu hapa kwetu. Nami ni mwongofu mpya na ninataka unitumie Biblia Takatifu moja na majorida pamoja na vitabu vya *Masih*. Nimepotea na kuonekana tena.

Bwana aibariki kwa wingi hudu-ma yako. Natumaini kusikia kutoka kwako punde.

Wako mtiifufu,

Mone Akinwa na familia
Jimbo la Sunshine, Nigeria



Mchungaji P.V.
Ratnam akisambaza
maandiko ya
Mchungaji Alamo
katika vijiji vya
Andhra Pradesh, India



HUDUMA YA MTANDAO YA ALAMO
www.alamoministries.com

roho iliyochukiza, kwani itabadili kweli ya MUNGU kuwa uongo! Pepo hili la ushoga lina nguvu, bali YESU, mbegu yenyenye uzima wa milele ndani YAKE, ana nguvu zaidi.⁷ MUNGU anatuambia tumpinge Shetani naye atatukimbia (Yakobo 4:7).⁸ Lakini serikali ya dunia husema kama tukiu pinga ushoga, tunafanya uhalifu wa chuki.

Kabla YESU hajapaa kurudi Mbinguni, ALIYASHINDA mauti, Kuzimu, Kaburi, Shetani, na mapepo yote ya upotovu, lakini yejote

akataaye uzima wa milele atafidiwa kwa maamuzi yake ya uovu.⁹ Watapokea ndani yao wenyewe malipo hayo ambayo ni Jehanamu na Ziwa la Moto, mateso milele. Wanajitendea haya wenyewe kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu (Luka 17:26-30).

Umekuwa ni mtindo kwa sasa kumfuata Shetani, ambaye amedanganya ulimwengu mzima (Ufunuo 12:9).¹⁰

Kile vinachofanya vyombo vyahabari na serikali wamelifanya

⁷ Kum. 4:39, 32:39, 1 Sam. 2:6-8, 1 Nya. 29:11-12, 2 Nya. 20:6, Zab. 46:1, Isa. 44:6, 45:23, Yer. 10:10, 18:6, Dan. 4:35-37, Yoh. 10:29, Mdo. 17:24-26, Ufu. 1:12-18 ⁸ Mat. 4:1-11, Rum. 12:9, Efe. 4:27, 5:3-17, 1 The. 5:21-22 ⁹ 1 Nya. 28:9, Ayu. 4:7-9, 21:14-20, Mit. 1:22-32, 8:36, 10:25, Isa. 1:15-20, Dan. 12:2-3, Lk. 12:4-9, Yn. 3:16-21, 36, Rum. 1:18, 1 Kor. 6:9-10, Yud. 14:15, Ufu. 20:11-15, 21:8, 27 ¹⁰ Mat. 24:11-12, 24, 1 Tim. 4:1-2, 2 Tim. 3:13, 2 Pet. 2:1-3, Ufu. 13:1-4, 11-15, 14:8, 17:8, 18:2-3, 23

Congo

(Imetafsiriwa kutoka Kifaransa)

Mchungaji wa Dunia Tony Alamo,

Amani katika Kristo! Mimi ni Mchungaji Andre Hilarion, mmoja wa wasomaji wakubwa ya Majarida yako. Ilikuwa mwaka 2006 wakati nilipogundua machapisho yako na yalibadili kabisa huduma yangu. Kwa maana Roho Mtakatifu aliyafungua macho yangu wakati nilipokuwa nikiyasoma. Kwa sababu hii, katika kanisa ambalo mimi ni mchungaji, sasa tunayatumia maandiko "Siri za Papa" kama chombo kwa ajili ya kushuhudia katika maeneo ya halaiki, na sasa Bwana anatenda mambo makuu. Kila juma tunapokea roho mpya ambazo zimeguswa na Roho Mtakatifu baada ya kusoma na kukubali, kwa kutoa mioyo yao kwa Yesu kuanza maisha yao mapya.

Hivyo, tunachoomba ni kwamba kwa upendo ututumie nakala nyingi zaidi pamoja na makala kwa lugha ya Kifaransa zitakazoturuhusu kutengeneza kituo cha usambazaji kwa ajili ya maandiko ya Tony Alamo.

Vinginevyo, Mchungaji Tony Alamo, Mungu wako ni Mungu wetu. Wito wako umekuwa wito wetu pia. Na mapambano yako ni mapambano yetu pia. Tunatanguliza shukrani zetu, na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu ili uwnejia ya baraka zaidi na zaidi kwetu na kwa watu wa kila taifa.

Andre Hilarion

Kimpese, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo

Missouri

Mpendwa Mchungaji Tony Alamo,

Nashukuru sana kwa ajili ya huduma yako na ufunuo wa kweli aliokupa Mungu. Kweli umefungua macho yangu na kuimarishe imani yangu katika Mungu, umebainisha kwangu udanganyifu wa Shetani, serikali za dunia, kazi zake dhidi yetu, Bibi harusi, na mengine yote yanayotumiwa naye katika ulimwengu huu uliopotea.

Tafadhali nitumie maandiko yote ambayo unatoa. Nayataka YOTE. Asante sana na Mungu aliye hai akubariki wewe na huduma yako kwa wingi na kuzidi katika neema yake na nguvu!

Tafadhali weka jina langu katika orodha yako ya maombi.

Katika Kristo,

Terry Birmingham

neno la mungu kuwa uhalifu wa chuki. Lakini hayo ndiyo maisha pekee na mbinu za kuepuwa kutoke kwenye maumivu makali na mateso ya milele katika Jehanamu na Ziwa la Moto. YESU na watu WAKE ndio pekee wanaojali roho yako. Usiiruhusu roho ya Shetani kukushawishi kwa namna nyininge yejote. Hukuzaliwa shoga. Pepo linawezakuwa lilikuwingia ulipokuwa mdogo sana, lakini YESU hufukuza mapepo toka kwa watu.¹¹ YEYE ni UZIMA na uzima tele.¹² "Mimi nilikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele" (Yohana 10:10).

Nikikuonyesha jinsi ya kuepuwa hukumu ya milele, utaamini kwamba huu ni uhalifu wa chuki. Maisha hapa ni mafupi, bali umilele ni mrefu.¹³ Hauna (Inaendelea ukurasa wa 4)

¹¹ Mat. 8:16-17, 28-34, 9:32-33, 10:1, Mk. 1:34, 39, 7:25-30, 9:17-27, 16:9, Lk. 11:14 ¹² Yoh. 11:25-26, 14:6

India

Mpendwa Mchungaji Tony,

Nilienda katika kijiji cha baba yangu kiitwacho Sandipudi siku kumi zilizopita kuona nyumba yetu ya zamani. Basi palikuwa na muumini aliyekuwa mgonjwa sana aliyekuwa amelala kwenye kitanda chake cha mauti na watu walidhani kuwa angekufa, lakini nilimtembelea na kumwombea. Mungu alisikia maombi na akamponya kabisa. Kupitia tendo hili mtaa mzima uliniheshimu sana, lakini nilisadiki na kuwaambia, "Si mimi, bali Yesu Kristo alitenda hili. Na tumpe Yeye utukufu na heshima."

Naamini kwamba sala zenu za thamani zilinisaidia katika huduma Yake. Hebu tumtukuze Yeye kwa matendo na maneno.

Asanteni nyote. Tafadhali niombeeni mimi na utume wetu zaidi.

Katika pendo lake,

Ndugu yako,

Rajesh Tatapudi

Andhra Pradesh, India

Cameron, MO

NJIA PEKEE YA KUTOKEA

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3) fufua siku ya mwisho.¹⁶ mwisho. Roho za watu zitaishi milele Mbinguni au Kuzimu.¹⁴ Upendo si ngono. Upendo ni kuzishika amri za MUNGU (1 Yohana 5:3).¹⁷ Kama ukifanya hivyo, Sote tu wanadamu. Sote tu mepewa haki ya kuchagua uzi-ma au mauti, mema au mabaya, kuwa ananijua MIMI (ananipenda) na hashiki amri ZANGU ni mwongo, na kweli haimo ndani yake (1 MUNGU au Shetani.¹⁵ ROHO wa Yohana 2:4). “Na kama walivyokataa kuwa na MUNGU katika fahamu zao, MUNGU aliwaacha wafuate

akili zao zisizofaa,” (maisha yao ya upotovu) wafanye mambo ambayo Shetani anataka wafanye, na roho wake mbaya ndani yao huwafanya wapende kufanya hivyo vilevile (Warumi 1:28-32).

Wapumbavu na wawe wafalme na kutawala dunia kwa dhahabu, upotoshaji, siasa, na mambo mengine, lakini moyo wangu ulete upendo usiozeeka.

(Inaendelea ukurasa wa 8)

¹⁶ Mk. sura ya 16, Yoh. 11:25-26, Mdo. 2:29-33, 4:10-12, 1 Kor. 15:3-22, 1 Pet. 1:3-5 ¹⁷ Kut. 20:6, Kum. 7:9, 11:1, 13-15, 30:16, Yos. 22:5, Yoh. 14:15, 21, 15:10, 2 Yoh. 6

Arkansas

Mpendwa Mchungaji Tony,

Leo nilikuwa na rafiki ambaye ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Alikuwa katika mazishi. Mtu aliyeureka alikuwa mhubiri, na kulikuwa na watu wengi kwenye mazishi yake. Ushuhuda wake kabla mauti haijamkuta ni kwamba popote alipokwenda, aliwaambia watu mara zote, iwe ni kwenye Walmart au kwenye ghala ya dawa au mtaani tu, “Je! Wamjua Yesu Kristo kama mwokozi wako binafsi? Je! Upo sawa na Mungu?” Alifanya hivi kila mahali alipokwenda, hadi ikafika hatua watu walijiuliza ni kwa nini alifanya hivyo.

Katika mazishi, binti yake alisimama na kusema, “nataka kuwaambia habari kamili kuhusu baba yangu. Nilipokuwa mdogo, yapata umri wa miaka 13, nilikuwa nikienda naye mara kwa mara, na kila mahali tulipokwenda alikuwa akisimama na kumuuliza mtu iwapo ameweke mambo yake sawa na Yesu, au angesema, ‘Je! Wamjua Yesu kama Mwokozi wako?’ Wakati mwingine nilihisi kuwa alizidi kipimo kufanya jambo hilo. Aliweza kumwambia kila mtu, na lilikuwa ni jambo endelevu.

“Siku moja tulipanda kwenye gari nami nilisema, ‘Baba, kwa nini unamwambia kila mtu kuhusu Yesu?’ Baba yangu alisema, ‘Binti, nitakwambia hadithi. Niliota ndoto namna ya maono nilipokuwa na umri wa miaka

17, na katika ndoto hiyo nilikufa na nikaenda Mbinguni. Ilikuwa ni sehemu nzuri mno. Kisha wakanichukua hadi kwenye kingo za Mbunguni, nami nikatazama chini kuelekea kuzimu. Niliona mikono hii ikiwa imeinulila kunielekea mimi na walikuwa wakinililia kwa uchungu, “Kwa nini hukutuambia! Kwa nini hukutuambia! Kwa nini hukutuambia!” Na walikuwa ni watu niliowajua. Ndoto iliisha na nikawa nimerudi duniani na hiyo ndio sababu namwambia kila mtu.”

Rafiki yangu alisema ilimfanya atukumbuke wengi wetu, kwa Maandiko ya Mchungaji Alamo, kwa sababu kila tuendapo, daima tunasambaza maandiko. Alisema Mchungaji Tony amekuwa akiwaonya watu kwa miaka na miaka.

Msifuni Bwana,
Ndugu Tommy

Kenya

Salamu Mchungaji Tony Alamo,

Nimenyong’onyezwa na swala lako. Nilibarikiwa sana na jarida lako “Nimempata Yesu kwenye Tovuti ya Tony.” Nilisoma makala na kusali kwa ajili ya msamaha kwenye jarida. Nilitubu dhambi zangu kwa dhati, kwa kweli nilitokwa na machozi kwani nilikuwa nikijutia muda wote niliopoteza duniani kumkufuru Mungu! Nilihisi kuondokewa na mzigo wa dhambi. Kwa hakika najisikia mwepesi na huru. Oh! Kweli nilikuwa nikikosa furaha ya aina hii, furaha ya kusamehewa dhambi, furaha ya kuishi katika Kristo. Namshukuru MUNGU kwa kuokoa roho yangu na ninaomba kwamba ROHO MTAKATIFU aniongoze katika safari hii ya kiroho. Sasa, nimeanza safari hii ya kiroho. Tafadhali niongoze jinsi ya kusonga mbele na kumwaibisha Shetani na uongo wake. Kwa mara nyininge tena nazishukuru huduma zako kwani zinatoa kila kitu kinachohusika na mahitaji yetu ya kiroho. Mungu akubariki wewe na huduma yako kwa uwingu na kuzidi

Sarah Terry

Bungoma, Kenya

Kutoka kwenye Idara yetu ya Kutafsiri

Tunafanya tafsiri za Ilacono (lughu inayozungumzwa kaskazini mwa Ufilipino), na mmoja wa watafsiri ni kijana mdogo ambaye alilelewa Kipentekoste, amehitimu kutoka kwenye seminari ya thiolojia, na mwalimu wa Shule ya Biblia kwa watoto. Kanisa lao lina makanisa mengine 50 yaliyosambaa mwote Kazakini mwa Ufilipino, kila moja likiwa na mchungaji wake. Kwa sasa anafanya kazi na American Bible Society akisaidia kutafsiri kila kitabu cha Biblia.

Alituambia kwamba alipoona hatimili kwenye "Siri za Papa," "Papa Mkimbizi," "Yesu alisema Shetani atakuwa na Kanisa na Serikali," na "Malkia wa Makahaba," aliona zikiwa na tarehe za miaka ya 80 na 90. Alisema inashangaza kwamba Mchungaji Alamo aliandika kweli hizi miaka mingi iliopita, na kwa wakati huo hakuna mtu aliyezeza kuona kwamba zilikuwa kweli, lakini sasa unawenza kuona kwa urahisi. Mchungaji Alamo alijua mambo haya kabla ya kila mtu na akayachapa ili kumuonya kila mtu.

Alisema Wafilipino ni Katoliki mno huwezi kuongea na hata mmoja wao kuhusu Bwana, lakini baada ya kusoma barua za watu wakiomba maandiko

ya kusambaza na watu wakishuhudia, aliomba nakala mia za kila andiko alilosaidia kutafsiri ili aweze kuyasambaza. Aliagiza lundo la vitabu vya Masihi pia. Alisema, "Natafsiri kwa ajili ya Jumuiya ya Biblia, lakini huu ni uongoaji wa roho." Alisema kuwa ana-jivunia kuwa sehemu ya huduma hii na anayatumia maandiko kwenye madarasa yake. Alisema, "nimekuwa kwenye Seminari na limo ndani yangu, lakini maandiko haya ni ya kweli na yanab-adili maisha. Naweza kuona umaana wa kile kinachoendelea kwenye maisha yangu binafsi. Naona maandiko haya ni jambo linalotokea sasa."

Mtafsiri wa Kiswahili ni mama wa watoto wawili ambaye mumewe ni mchungaji. Alisema ilimpasa kuwa mwamini, kiasi kwamba alipokuwa akifaya kazi kwenye vipande vya maandiko kuhusu papa, alidhani baadhi ya shutuma dhidi ya papa na Kanisa Katoliki zilikuwa uzushi na kukuza mambo. Alisema kuwa alifa-hamu kwamba Ukatoliki ni mafundisho ya uongo, hivyo ukweli wa ujumbe haujalishi kwani unawafanya watu waugeuke. Lakini bado, hakuuamini.

Alisema mume wake alikuwa akisoma nakala za Tony Alamo usiku mmoja na akamuuliza, "Kwa nini uliagiza hizi?" Akmjibu, "Ili niweze kuwapa watu ninapowapeleka watoto mbugani." Kwa haraka alisema, "Kwa hakika hapana! Uzihifadhi! Maandishi haya ni ya muhimu sana. Mambo haya ni ya kweli! Inabidi tuyasome." Alisema, "Nilikwenda kwenye chuo cha Biblia na mambo haya yanafundishwa na yamo kwenye nyaraka na kila lililoandikwa humu ni la kweli."

Anasema alimtzama mume wake na kujisemea moyoni, "Ulikwenda kwenye chuo cha Biblia miaka ya nyuma na ulijua kwamba mambo haya ni ya kweli. Umefanya nini au chuo kimefanya nini kuuonya ulimwengu? Si wewe wala mtu mwingine yeoyote amefanya chochote kuhusu jambo hili. Mtu huyu (Mchungaji Alamo) ameitwa na Mungu kuongea kwa sababu hakuna mtu mwingine, ikiwa ni pamoja na wewe, amefanya hivi au atafanya." Alisema, "Naamini jambo hili sasa, na nachukizwa na wale hawakusema ukweli, lakini waliuficha."

Mtafsiri wa Kiswedishi alikulia kwenye Uprotestanti, lakini kwa miaka mingi hakujishughulisha kabisa na mambo ya kanisa, dini, au Mungu. Yeye ni mwanaharakati wa siasa, akipambana na makosa ya serikali ya Swedeni. Anaandika machapisho ya kisiasa kwenye blogu, ana mikutano na anatafsiri maandiko kwa lugha yake. Ana uhakika na imani zake, lakini aliposomaaya chache za kitabu cha Masihi, alianza kulia alipokuwa akisoma, "Kundi lilipiga kelele, 'Asulubiwe, Asulubiwe'."

Alituambia, "Nimejifunza nadharia mbalimbali za njama, lakini sijawahi kuona yeoyote akizihusisha na Vatican kama hivi. Inashangaza. Napenda kweli kufanya hivi. Nyote mnaanza kunishawishi. Nilikuwa nikiandika blogu yangu na nimejikuta nikanukuu Ufunuo."

Mtafsiri wa Kiserbia, ambaye ana shahada ya historia, alisema inasisimua kuwa sehemu ya huduma hii. Alisema Historia ya Serbia imejawa na mateso ya kidini na mauaji mengi, na Mchungaji Alamo anapata mateso ya kidini na bado anaendelea kuongea. Alisema hili ni jambo la kusimua.

Nigeria

Wapendwa Huduma za Alamo,

Salamu kwenu katika jina la mbarikiwa Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Jarida la Huduma za Kikristo za Tony Alamo kwa kiasi kikubwa linabadili maisha ya watu wa Mji wa Igodan Lisa katika Nigeria. Upako katika jarida hili ni mkuu sana. Limenisaidia katika maisha yangu ya kiroho kwa kuniinua katika ngazi mpya ya uelewa wa mambo ya Mungu. Alikuwa ni msambazaji ndiye aliyenipa jarida lako lenye kichwa cha habari "Tetemeko la ardhi." Nilitumia fursa hiyo pia kuwafikishia watu wengine na kila niliyempa karatasi hilo, walimpokea Yesu kama Bwana wao. Utukufu, sifa ziwe kwa Mungu.

Tafadhalni nakuomba ututumie mengine zaidi, ili yaweze kutusaidia kuzileta nafsi kwa Mungu. Mungu abariki kazi zako. Asante.

Wako katika Kristo,
Jasaau Imamu

Jimbo la Ondo, Nigeria

New York

Ndugu Mchungaji Tony Alamo,

Nilipokea jarida lako nikiwa katika treni ya chini kwa chini Jijini New York, na liliuja kwangu wakati nilipokuwa nikilihitaji sana. Habari zilizomo kwenye jarida lako ni za muhimu sana.

Pia naomba kitabu chako cha *Masihi*, majarida 100, pamoja na ujumbe katika CD.

Asante,
Eric F.

Rhinebeck, NY

Ushuhuda wa Uponyaji

(Imetafsiriwa kutoka Kireno)

Oktoba 27, 2014

Jina langu ni Mchungaji Isaque Roberto. Natoka Londrina katika Jimbo la Paraná, Brazil, na Ningependa kuwashirikisha jambo kupitia barua pepe hii. Nimekuwa mchungaji Londrina kwa miaka 15. Miaka mitatu iliyopita familia yangu ilihuzunishwa na maafa ambayo yalibadilika kuwa tukio kubwa.

Tarehe 24 Julai, 2011, binti yetu Beatriz Gabriela (akiwa na umri wa miaka saba), alipata ajali mbaya barabarani alipogongwa na dereva wa teksi alipokuwa akitembea kwenye kivukio cha wapita njia. Athari ya ajali ilikuwa kubwa kiasi ambacho, kwa mujibu wa wakagazi, alitupwa mbali takribani futi 21. Nilikwenda mbio upande alipokuwa, alikua hana pumzi, na nakumbuka nikipiga mayowe, "Mtu ye yote aniitie msaada!" Nilipomtazama tena, niliona gurudumu la pipipiki na sauti iliyosema, "Nitakusaidia. Mimi ni mzima moto." Kwa wakati ule, Mungu alitoa jibu la kwanza pale. Alimla za Beatriz kifudifudi na kujaribu kumrudishia fahamu, akakoho damu. Msaada uliwasili, na walipokuwa wakimshughulikia ndani ya gari la wagonjwa, nikaanza kuomba. Ibilisi naye alikuwa akikabiliana nami huku akinionyesha akilini taswira ya mvulana niliyemfahamu ambaye aligongwa na gari akapoteza uwezo wa kuongea na uratibu wake. Kwa sasa familia yake wanambeba kwenye kiti cha magurudumu. Kwa wakati ule, ibilisi alikuwa akiniletea taswira yake akisema, "Hivyo ndivyo binti yako ataka vyokuwa."

Beatriz alipeclekwa hospitali na kulazwa akiwa na vipimo vifuatavyo: amevunjika mguu wa kushoto, amevunjika mkoно wa kushoto, amevunjika mtulinga wa kulia na kushoto, bandama imekatwa sana,



mapafu yameharibika na jeraha la kichwa la ngazi ya 3 (ngazi ya 4 ni kifo).

Tulipofika kwenye kitengo cha wagonjwa mahututi, tulimwona binti wetu akiwa ameunganishwa na vifaa kadhaa, akipumulia mashine, na akiwa amezimia. Siku tatu baada ya ajali, Julai 27, daktari wa upasuaji wa akili aliyekuwa akimhudumia alituita na kusema, "Sina habari njema. Hali yake imezidi

kuwa mbaya zaidi. Beatriz hasaidiki na dawa alizopatiwa, na amepata uvimbe kwenye ubongo. Kutokana na hali hiyo, damu haizunguki kupita kwenye ubongo, na ndani ya saa chache zijazo ubongo wa Beatriz utakuwa umekufa." Daktari alisema, "Nina mbadala, ambao ni kufanya upasuaji kuondoa kipande cha fuvu kila upande ili kupunguza shinikizo kwenye ubongo wa Beatriz, hivyo utakuwa na nafasi ya kutanuka. Hata hivyo, hakuna uhakika kwamba hali yake itabadilika au anaweza kuhimili upasuaji."

Tuliidhinisha upasuaji, kwa sababu tulijua kwamba neno la mwisho lili-kuwa ni la Mungu. Walipokuwa wameandaa kila kitu tayari, walituambia tukae na Beatriz ili tuweze kumuaga. Mke wangu alianza kuomba nilipoku-

wa nikiwaita waombaji wengine na kuwaelezea hali halisi. Mke wangu alipokuwa mbele ya Beatriz akiomba, mtu mmoja alimjia na kusema, "Mama, nakushauri umwombee Mungu amchukue, kwa sababu ikiwa atafani-kiwa kuishi, atakuwa tu mtu wa kulala kitandani." Saa chache baadaye, bila kujua kilichotokea, nilipokea ujumbe kwenye simu yangu kutoka kwa shemeji yangu (wa-kike) ambaye alisema alikuwa akiomba wakati wa mchana na alipata maono. Aliona pepo wabaya wakimjia mke wangu na kusema maneno yale yale.

Upasuaji ulidumu kwa takribani saa tano. Walipomleta Beatriz kwenye chumba cha wagonjwa mahututi, kichwa chake chote kilikuwa kimefungwa bendeji na uso wake ulikuwa umeharibika. Sasa ikawa ni kusubiri tu. Tulimwomba Mungu amponye, lakini habari mbaya ziliendelea kuja – nimo-nia, maambukizi ya hospitali.

Siku moja kabla ya siku ya kuzaliwa ya Beatriz (Agosti 8), daktari alisema angemtoa kwenye kitulizo kuona kama angeweza kuzinduka kutoka kwenye hali ya kuzimia. Niliuliza, "Unadhani itamchukua muda gani kuamka?"

"Hakuna namna naweza kujua kwa hakika," alisema. "Anaweza kuamka leo, kesho, wiki ijayo, mwezi ujao, mwakani, lakini pia anaweza asiamke tena," alihitimisha.

Siku chache baadaye, vifaa vya msaada wa kupumua viliondolewa. Tulianza kushereheka kwa sababu alianza kuamka. Hata hivyo, wakati wa usiku Beatriz alikua amemeza mate yake wakati akipumua. Tulipofika hospitali, tulimwona akiwa anapumua kwa shida sana. Timu ya matibabu waliikuwa wakifanya yote waliyoweza kumrejesha katika hali nzuri zaidi. Tilitoka kwenda kupata chakula cha mchana,



na tuliporudi na kuomba kuingia ndani, tulizuiliwa. Nilichungulia kuptitia kwenye mlango na nikaona karibia timu nzima ilikuwa imezunguka kitanda chake ikiwa inalia. Ilitubidi tusubiri dakika kadhaa, na tuliporuhusiwa kuingia ndani, tuliona kwa mara nyingine Beatriz amewekewa bomba la kupumulia. Mmoja wa madaktari alisema, "Iletubidi kumwekea bomba la pumzi, na Beatriz atatakiwa kuvuta oksijeni yake kwa kutumia bomba. Hakuwa na uwezo wa kuvuta pumzi yake mwenyewe." Habari mbaya zaidi – sababu nyingine ya kuomba. Siku kadhaa baadaye, Beatriz alizinduka kutoka kwenye hali yake ya kuzimia na akapelekwa sehemu ya wagonjwa.

Tuliendelea kumlilia Mungu na kufunga muda wote. Wakati Beatriz alipokuwa sehemu ya wagonjwa, tulibadili chumba kile kuwa kituo cha maombi, saa 24 kwa siku. Tulikuwa na nyimbo za kuabudu zikicheza. Tuliomba kila saa. Watu waliingia ndani na kumwona Beatriz akiwa amelala kitandani miguu yake ikiwa imefungwa bendeji, amefungwa mashine za kupumulia na za kulishia na wakasema, "Pawezaje kuwa na imani kiasi hiki mahali hapa?" Kwa pamoja kulikuwa na siku 53 za kulazwa hospitali.

Wakati Beatriz aliporuhusiwa kutoka hospitalini, alifika nyumbani bila kuonyesha dalili yoyote ya kupata nguvu tena. Tulikuwa na kitanda cha hospitali, kiti cha kuogea, na kiti cha gurudumu nyumbani. Mke wangu alikuwa akizungumza na mtaalamu wa mazoezi ya viungo na kumuuliza, "Daktari, unadhani itachukua muda gani Beatriz kuweza kutembea?" Daktari akajibu, "Kwa miaka ambayo nimehudumu katika udaktari, sijawahi kuona katika maandishi yoyote ya kitabibu au kusikia habari yoyote ya mtu yeyote aliywahili kupona kwenye ajali kama aliyopata Beatriz. Labda siku moja anaweza kutembea kwa kutumia magongo au mtu wa kumshika akitembea, lakini kuweza kutembea tena kawaida – kwa maoni yangu – kamwe haiwezekani tena." Hata hivyo,

tulidhamiria katika roho zetu kwamba asiishie katika hali hiyo. Imara tuliendelea kumtafuta Bwana, wakati mwingine katika imani, wakati mwingine tukilia, lakini mara zote tuliamini. Siku moja tulimchukua kwenye kliniki ya jamii kwa sababu tulihitaji rufaa, na nilimwambia daktari kwamba ilikuwa ni jambo la haraka. Daktari aliomba kumwona Beatriz, na nilipotembea kuingia ofisini nikiwa nimembeba mikononi mwangu, daktari aliuliza, "Bw., kwa nini una haraka kiasi hicho? Nini kinaweza kubadilika katika hali ya mtoto huyu?"

Beatriz alilazimika kufanyiwa upasuaji kuwekewa chombo bandia mahali mfupa wa fuvu uliondolewa. Tulipata makisio ya (Real za Kibraili) \$147,500.00 (karibia \$60,000.00 Dola za marekani). Hatukuwa na pesa, hivyo tulikuwa na sababu nyingine ya kuomba. Tukiwa tumepokea maelekezo kutoka kwa Mungu kuptitia rafiki, tulianza kampeni ya kupata pesa. Siku ya Alhamisi, nilipokea simu. Alikuwa ni mwanamke aliyeanza kuuliza maswali kuhusu Beatriz. Aliuliza ni kiasi gani tulichohitaji bado, nami nikasema (BRL) \$57,000.00 (23,000.00 Dola za marekani). Alisema kwamba ataangalia kama anaweza kutusaidia. Jumatatu iliyoauta, nilipokwenda benki kuangalia salio, niligundua kwamba mtu yule alikuwa ameweka kiasi cha fedha tulichokuwa tunahitaji. Ndani ya siku 40 tuliweza kupata kila sarafu tuliyokuwa tunahitaji. Bwana Asifiwe!

Upasuaji ulifanyika tarehe 23 Desemba, 2011. Kwa wakati huo, Beatriz tayari alikuwa anaweza kukaa kwa msaada wa mito na aliweza kukaa kwenye kiti cha magurudumu. Tarehe 27, Desemba nilikwenda kusema kwaheri kwa Beatriz kabla ya kuondoka kwenda kanisani. Nilishika mikono yake na kumwambia kwamba nilikuwa nakwenda kanisani. Mara nikamsikia akivuta mikono yangu. Nilimshika kwa nguvu na mara ya kwanza akasimama. Niliogopa na kurudi hatua nyuma, na kwa wakati huo huo, ali-piga hatua moja mbele na akaendelea kutembea. Mungu ni mwaminifu!

Siku zilivvosonge mbele, Beatriz aliendelea kurejeza uwezo wake. Alianza kuongea na kuandika. Katika mwezi Mei 2012, alirudi shulenii.

Leo, miaka mitatu baadaye, yeye ni ushuhuda hai wa muujiza, usiowenza kueleweka, uthibitisho kwamba Mungu ni mwaminifu kwa Neno Lake na anawajibu vyema wale wote wanaoamini. Neno ambalo ninalo kwa ajili ya maisha yako wakati wote ni, "KILA JAMBO LINAWZEKANA KWAKE AAMINIYE" (Marko 9:23).

Siku chache zilizopita, mke wangu alikuwa na mtaalamu wa mazoezi ya viungo, na daktari alikuwa akimwonyesha Beatriz kwa mmoja wa wanafunzi wake na akasema, "Huu ni muujiza, kwa sababu kama isingalikuwa Mungu, asingekuwa (Beatriz) hapa. Hapakuwa na dawa ya kuweza kumponya."

Dawa haikuweza kufanya chochote, lakini MUNGU ANAWEZA! ANAWEZA KUFANYA KAZI MAISHANI MWAKO PIA!

Mchungaji Isaque Roberto

Ushuhuda huu umeshirikishwa na kanisa zima katika Londrina na umekuwa mfano wa nguvu ya Mungu kutupa changamoto, katika imani yetu. Tazama ushuhuda ambao tumerekodi kanisani kwenye You Tube: <http://www.youtube.com/watch?v=YHqbBk0A4nA>.

Cuba

(Imetafsiriwa kutoka Kihispaniola)
Salamu kutoka Cuba,

Amani ya Bwana iwe na kila mmoja. Shukrani kwa Bwana, leo tulikuwa na baraka za kupokea vifurushi viwili zaidi.

Toa shukrani zetu kwa watumishi wote wa Mungu ambao wana baraka za kupeleka Neno kwa ulimwengu wote kuptitia huduma hii.

Mungu akubariki,
Mchungaji Marrero Havana, Cuba

NJIA PEKEE YA KUTOKEA

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 4)

Pokea mbegu ya maisha yasiyo na mwisho. Anza kwa kusali sala hii:

BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mwenye dhambi¹⁸ ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.¹⁹ Ninaamini kwamba alikuwa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.²⁰ Ninaamini kwamba MUNGU alimfufua YESU kutoka kwa wafu kupidia nguvu za ROHO MTAKATIFU²¹ na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikiliza maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.²² Ninafungua mlango wa moyo wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.²³ Nioshe dhambi zangu kwa damu uliomwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,²⁴ hutani-kataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia linasema hivyo.²⁵ NENO LAKO linasema

hutamkataa yeote na mimi nikiwemo.²⁶ Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.²⁷ Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kutotenda dhambi tena.²⁸

BWANA anataka uwaambie wengine juu ya wokovu wako (Marko 16:15). Unaweza kuwa msambazaji wa maandiko ya Injili ya Mchungaji Tony Alamo. Tutakutumia maandiko bure bila gharama. Tupigie au tutumie barua pepe kwa maelezo zaidi. Shiriki ujumbe huu na mwinge. Baada ya kuokoka YESU alisema ni lazima kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa kwenye maji mengi kwa jina la BABA, MWANA na ROHO MTAKATIFU.²⁹ Kwa makini soma Biblia ya KJV, tafsiri ya Kiswahili ya The Bible League, Waenezaji wa Neno la Mungu tangu 1938 na ufanye inavyosema.³⁰

BWANA anakutaka uwaambie wengine kuhusu wokovu wako. Unaweza kusambaza makala ya Injili ya mchungaji Tony Alamo. Tutakutumia makala hizi bila malipo. Tupigie simu ama ututumie barua

pepe kwa habari zaidi. Mshirikishe na mtu mwinge ujumbe huu.

Iwapo unataka dunia yote iokolewe, kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, “Je! Mwanadamu atamwibia MUNGU? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghallani, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa MAJESHI; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeze alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema BWANA wa MAJESHI. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema BWANA wa MAJESHI” (Malaki 3:8-12).

¹⁸ Zab. 51:5, Rum. 3:10-12, 23 ¹⁹ Mat. 26:63-64, 27:54, Lk. 1:30-33, Yoh. 9:35-37, Rum. 1:3-4 ²⁰ Mdo. 4:12, 20:28, Rum. 3:25, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 5:9 ²¹ Zab. 16:9-10, Mat. 28:5-7, Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21, 10:17-18, 11:25, Mdo. 2:24, 3:15, Rum. 8:11, 1 Kor. 15:3-7 ²² Lk. 22:69, Mdo. 2:25-36, Ebr. 10:12-13 ²³ 1 Kor. 3:16, Ufu. 3:20 ²⁴ Efe. 2:13-22, Ebr. 9:22, 13:12, 20-21, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 1:5, 7:14 ²⁵ Mat. 26:28, Mdo. 2:21, 4:12, Efe. 1:7, Kol. 1:14 ²⁶ Mat. 21:22, Yoh. 6:35, 37-40, Rum. 10:13 ²⁷ Ebr. 11:6 ²⁸ Yoh. 5:14, 8:11, Rum. 6:4, 1 Kor. 15:10, Ufu. 7:14, 22:14 ²⁹ Mat. 28:18-20, Yoh. 3:5, Mdo. 2:38, 19:3-5 ³⁰ Kumb. 4:29, 13:4, 26:16, Yos. 1:8, 22:5, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Yak. 1:22-25, Ufu. 3:18

Tafadhalii wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambazo unaweza kuvutiwa nazo:

Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078

Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362

www.alamoministries.com • taoffice@alamoministries.com

Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani amba wanataka kumtumikia BWANA kwa miyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.

Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.

Tafadhalii wasiliana nasi kupidia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.

Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kitiwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO

alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.

Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kupidia meli.

Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhalii tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)
USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

Kwa wale ambaa mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo mtachapisha tena, tafadhalii jumuisha haki hii na usajili: